

MKATABA WA MAUZIANO YA SHAMBA

104

Mkataba huu unafanywa leo tarehe **19 Mwezi Oktoba, Mwaka 2018**

KATI YA

SALOME D YAREDI wa **S.L.P 1249 Dodoma** ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **"MUUZAJI"** neno ambalo litamjumuisha yeye mwenyewe, mwanasheria wake, wakala wake, warithi wake na yeyote atakayedai haki kupitia kwake kwa upande mmoja.

NA

LAND NETWORK LIMITED wa **S.L.P 3118 Dodoma** ambayo katika mkataba huu itajulikana kama **"MNUNUZI"** neno ambalo litajumuisha yenyewe, mwanasheria wake, wakala wake, warithi wake na yeyote atakayedai haki kupitia kwake kwa upande wa pili

KWA VILE "MUUZAJI" ni mmiliki halali wa shamba lenye ujazo wa **Ekari nne tu (4 acres)** lililopo **Mtaa wa Chilwanha, Kata ya Ihumwa Wilaya ya Dodoma Mjini, Mkoa wa Dodoma.**

NA KWA VILE "MUUZAJI" kwa hiari yake mwenyewe na bila kushawishiwa au kushurutishwa na mtu yeyote anania ya kuuza na **Mnunuzi** kwa hiari yake na bila kushawishiwa au kushurutishwa na mtu yeyote anapenda kununua shamba tajwa hapo juu na lisilo na mgogoro wowote au lisiloweza kuleta mgogoro wowote hapo baadae, kwa kiasi cha fedha, masharti na makubaliano kama yanavyoonekana kwenye mkataba huu.

MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO:-

1. Eneo ambalo **Muuzaji** anamuuzia **Mnunuzi** lina ujazo **Ekari nne tu (4 acres)** lililopo **Mtaa wa Chilwanha, Kata ya Ihumwa Wilaya ya Dodoma Mjini, Mkoa wa Dodoma**, mipaka yake ni kama ifuatavyo:-

- 1.1 Mashariki linapakana na **ALFRED MWALUKO**
- 1.2 Magharibi linapakana na **SALOME MWALUKO**
- 1.3 Kaskazini linapakana na **GODFREY MWALUKO**
- 1.4 Kusini linapakana na **ELIZABETH FADE**

- 2 Kwamba **Muuzaji** anauza shamba lenye ujazo wa **Ekari nne tu (4 acres)** lililopo **Mtaa wa Chilwanha, Kata ya Ihumwa Wilaya ya Dodoma Mjini, Mkoa wa Dodoma** na **Mnunuzi** ananunua shamba tajwa hapo juu kwa bei ya fedha za kitanzania shilingi **Milioni mbili na laki moja tu (Sh 2,100,000/=)** ambazo katika mkataba huu zitajulikana kama **"bei ya shamba"**

- 3 Kwamba kiasi cha **bei ya shamba**, fedha za kitanzania shilingi **Milioni mbili na Laki moja** tu (**Sh 2,100,000/=**) zinalipwa siku ya kusaini mkataba huu; na kwa kusaini mkataba huu **MUUZAJI** anakiri kupokea kiasi cha fedha tajwa hapo juu.
- 4 **Muuzaji** anakabidhi kwa **Mnunuzi** haki zote na vielelezo vyote vinavyohusiana na miliki ya shamba tajwa hapo juu baada ya kupokea malipo tajwa.
- 5 Pale ambapo mkataba huu utasitishwa au kufahamika kuwa haufai kwa sababu **Muuzaji** sio mmiliki halali wa shamba tajwa hapo juu na au shamba tajwa lina mgogoro, pande hizi mbili katika mkataba huu zitajiridhisha kuvunja mkataba huu, na pesa zilizokwisha tolewa awali au zilizokwisha lipwa kwa ukamilifu wa bei ya shamba zitarudishwa kwa **Mnunuzi** mara moja pamoja na gharama nyingine za usumbufu zitakazo kokotolewa na **Mnunuzi**, na kwamba kama **Muuzaji** hatakuwa tayari kurudisha fedha hizo, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
- 6 **Muuzaji** anakiri kuwa, shamba tajwa hapo juu halina mgogoro wowote, na pale itakapotokea kwa shamba hilo likazua mgogoro unaotokana na misingi ya umiliki uliokuwa wa **Muuzaji**, basi **Muuzaji** ataukabili mgogoro huo na kuhakikisha umekoma bila kumpa adha **Mnunuzi**.
- 7 Mkataba huu unalindwa na kusimamiwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

MKATABA HUU unatiwa sahihi na wahusika pande zote mbili kama inavyoonekana hapa chini:-

Umesainiwa Hapa Dodoma na **SALOME D YAREDI**
aliyetambulishwa kwangu na *Samwel Ikwabe*
ninayemfahamu vizuri leo tarehe 19 Mwezi Oktoba, 2018



.....
MUUZAJI

MBELE YANGU:

Sahihi:


Jina: EZEKIEL AMON MWAKAPEJE

Anuani: 11058, DODOMA

Wadhifa: WAKILI



Umesainiwa na kuwekwa Lakiri ya **LAND NETWORK LTD**
ambaye ni **Mnunuzi** hapa Dodoma, mbele yangu,
leo tarehe 19 Mwezi Oktoba, 2018.



MBELE YANGU

Jina: SAMWEL JOEL IKWABE

Sahihi:.....

Anuani: S.L.P 3118 DODOMA

Cheo: MKURUGENZI

Mkataba huu umeshudiwa na Uongozi wa Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:-

Jina: EMMANUEL MANYIKA

Sahihi:

Anuani: S.L.P. 1249 CHILWANHA, DODOMA

Cheo: MWENYEKITI WA SERIKALI ZA MTAA/ KIJJI

